https://dspace.org/

Hongera Ni Ungonooro; Ifikiriwe ena Maana Yake Kenye Makamusi Ya Kileo

Karama, Mohamed

2024
East African Journal of Swahili Studies
http://ir-library.kabianga.ac.ke/handle/123456789/892
Karama, M. (2024). Hongera Ni Ungonooro; Ifikiriwe ena Maana Yake K enye Makamusi Ya Kileo. East African Journal of Swahili Studies, 7(1), 416-428. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2258.

Downloaded from a DSpace repository. https://dspace.org/

East African Journal of Swahili Studies, Volume 7, Issue 1, 2024
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2258

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 7, Issue 1, 2024
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

Original Article

Hongera Ni Ungonočoro; Ifikiriwe Ṭena Maana Yake K̇enye Makamusi Ya Kileo

Mohamed Karama[1*]

[1] Chuo Kikuu cha Kabianga, S. L. P. 2030 – 20200, Kericho, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0003-2341-9966; Barua pepe ya mawasiliano: mkarama@kabianga.ac.ke

DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2258

Tarehe ya Uchapishaji:

01 Oktoba 2024

Istilahi Muhimu:

Hongera, Pongezi, Maneno Mwiko, Uṭamaḍuni, Kamusi, Kungwi.

IKISIRI

Mabaḍiliko ya kisemantiki ni haliya isiyopingika katika ukuwaji wa luğa yoyoṭʰe ulimwenguni. Pahala pamoja ambapo maneno huhifaďiwa k̇a matumiyaji ya sasa na ya vizazi vijavo ni makamusini. Makamusi hukusanya maana za mingi ya maneno yanayotumika katika jamii na k̇amo mabaḍiliko ya kisemantiki hujiṭokeza. Makala haya yamelenga kuṭaťmini maana ya neno “hongera” k̇enye makamusi ya kiSwahili ya awali na ya kileo minṭarafu ya uṭamaḍuni wa waSwahili, wekahazina wa luğa ya kiSwahili. Maďumuni ya uṭafiṭi wetu yalikuwa kučanganuwa maana ya neno hongera kama msamiyaṭi k̇enye makamusi; kučunguza maana ya neno hongera katika mila za waSwahili; na kuṭaťmini uwafiki wa matumiyaji mapana ya neno hongera katika jamii leo. Naďariya ya Usemezano, iliyoongoza uṭafiṭi huu, inafafanuwa kuwa maana haswa ya neno hupatikana k̇a k̇angaliya vigezo va usuli, mapisi, mukṭaďa, sajili, uṭamaḍuni, ainaṭi za luğa zilizomo k̇enye lugha hiyo; la ṣivo, tuṭapata maana ya kijuujuu au ya kikamusi. Data yetu tuliikusanya k̇a kuwauliza, kupiṭiya mahojiyano yasomuunro, wasailiwa 5 wa marika zetu (wa miyaka 55 k̇enra chini) na piya wazee 5 (wa miyaka 70 na zaiḍi) kuhusu usuli, mukṭaďa wa matumiyaji, na mafafanuzi ya kiṭamaḍuni juu ya neno hilo “hongera”. Aiďan maaṇḍiko ya waṭaalamu na makamusi yenye ťika piya yalipitiwa na kučanganuliwa ili kutupa data ya neno “hongera”; kupunguza mlemeyo wowoṭʰe wa wahijowa; na piya kuhakikiša mayelezo ya wasailiwa. Uṭafiṭi wetu ulițibiṭiša kuwa hongera latumika k̇a maana ya “ku-pongeza” ṭu k̇enye makamusi ṭajika ya kiSwahili sanifu ya kileo, k̇a mfano, *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2016). Awali, katika makamusi asasi ya Krapf (1882) na Sacleux (1891/1939), maana ya hongera imeťubuṭu kumaaniša awamu katika šerehe ya ṭohara au ni kufariji k̇a mikasa iliyompata mtʰu. Aiďan, maṭokeyo yetu yaligunruwa kuwa “hongera” ni neno limaanišalo “pʰole” katika kiSwahili Asiliya (lahaja za ṗani Afrika Mašariki) lakini maana hii imevunjwa na maana ya kiṭamaḍuni k̇a sababu ni awamu katika šerehe ya ṭohara, piya ni awamu katika šerehe ya harusi ya kiSwahili haswahaswa wakati wa ḃanaharusi k̇ingiya nrani kuwonana na biharusi kimwili. Kimila ya waSwahili neno hili ni ṁiko wa daraja ya juu—lahusu ngono—hivo hwanika ungonočoro linapotumika pasipo. Lengo la uṭafiṭi huu ni kušauri ifikiriwe ṭena maana ya neno hongera katika makamusi ya

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

kileo. Uṭafiṭi huu una naṭija k̇a wanaleksikografiya kufanya uṭafiṭi zaiḍi wanapotengeza makamusi. Piya uṭawafaa wanaiḍara ya uṭamaḍuni katika mamlaka kujuwa asili na mila za watumiyaji wa luğa hii ya kiSwahili na nyenginezo ṇčini.

APA CITATION

Karama, M. (2024). Hongera Ni Ungonočoro; Ifikiriwe Ṭena Maana Yake K̇enye Makamusi Ya Kileo. *East African Journal of Swahili Studies*, *7*(1), 416-428. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2258.

CHICAGO CITATION

Karama, Mohamed. 2024. "Hongera Ni Ungonočoro; Ifikiriwe Ṭena Maana Yake K̇enye Makamusi Ya Kileo". *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 416-428. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2258

HARVARD CITATION

Karama, M. (2024) "Hongera Ni Ungonočoro; Ifikiriwe Ṭena Maana Yake K̇enye Makamusi Ya Kileo", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 416-428. doi: 10.37284/jammk.7.1.2258

IEEE CITATION

M.. Karama "Hongera Ni Ungonočoro; Ifikiriwe Ṭena Maana Yake K̇enye Makamusi Ya Kileo", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 416-428, Oct. 2024.

MLA CITATION

Karama, Mohamed. "Hongera Ni Ungonočoro; Ifikiriwe Ṭena Maana Yake K̇enye Makamusi Ya Kileo". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, Oct. 2024, pp. 416-428, doi:10.37284/jammk.7.1.2258.

UTANGULIZI

Ṭahaďari: Makala haya yanaomba samahani kuṭokana na luğa nzitʰo na ya wazi isotumiya ṭasfiḍa wakaṭi wa mayelezo na mafafanuzi yake kuhusiyana na ungonočoro au ungonografiya.

Katika ṁaka 2011 au karibu na hapo, wanabodi wa Research Institute of Swahili Studies of Eastern Africa (RISSEA), iḍara katika Makumbušo ya Kenya, nami ni mṭafiṭi katika ṭaasisi hiyo, walituṭembeleya na kutušajiiša katika tuyafanyayo k̇a faiḍa ya elimu na jamii. Awali, alisimama profesa mmoja akatupa "hongera", k̇a kuliṭaja neno hilo, k̇a kazi nzuri ṫifanyayo. Profesa T.S.Y Sengo, Mungu atuwekee mzee wetu, ṁanabodi vilevile, aliposimama yeye k̇anza alimsahihiša na kumkemeya profesa huyu k̇a kutumiya neno "hongera" k̇a maana ya kutupa pongezi. Wakaṭi huwo mimi na wenzangu, vijiṭafiṭi, hatukusubuṭu haṭa kumuuliza mzee k̇a nini lisitumike neno hilo k̇a maana ya pongezi. Fikira zetu zikapiga yaonekana kuna maana ya baṭini ambayo haṫijuwi na hatukuuliza lakini nripo uṭafiṭi wetu ulipoanziya kuṭaka kujuwa.

Tufululize haḍi ṁaka huu, 2024, ṫasoma ḍarasani *Mhanga Nafsi Yangu* (2015) kiličoaṇḍik̇a ni Said Ahmed Mohamed (SAM), Mungu piya atuwekee mzee wetu, Mpʰemba (k̇a kukisema kiPʰemba kik̇awo) kulingana na utangulizi wa Profesa K.W Wamitila katika *Jicho la Ndani* (SAM, 2002, uk. xiii), na ṫakuta maana ṭafauṭi ya neno "hongera". Kama tuṭakavokuja kubainiša baaḍaye katika makala haya, tulipokisoma kifungu hičo k̇a makini nripo iliponifunukiya mimi k̇a nini Profesa Sengo ali(m)kataza utumiyaji ya neno "hongera" k̇a maana ya "pongezi" k̇enye kikao hičo RISSEA. Tuṭanukuu kifungu hičo k̇a ukamilifu ili mukṭaďa uweleweke vizuri. Katika *Mhanga Nafsi Yangu* ukurasa 149-150 čapa ya 2015 ṫanukuu:

Tukija katika upande wa arusi yenyewe, jambo nililonifanya niichangamkie arusi yenyewe ya uongo na ukweli, nilikumbushika arusi ya Motoni [uSwahilini] – arusi za ndovu kumla mwanawe. Zingeanza kuchumbia kwa vuguvugu la ndani kwa ndani na kulishia. Zikafuata posa kupitia mshenga. Kisha utafiti wa kina juu ya mwelekeo wa mposaji na anayeposwa. Halafu kutajwa mahari kwa kushangiria. Baadaye kulipwa mahari kwa vigelegele na hoihoi. Tena kuna kualika arusi pande mbili, kuukeni na kuumeni – jambo linalotaka makini ya kutomsahau na kumwacha mtu wa karibu na wa mbali. Kisha hekaheka za kununua: nguo na mapambo ya bibi na bwana arusi, samani na vifaa vya nyumba yao, vinywaji na vyakula mbalimbali kwa sherehe. Tena kuna shinda [ushinzi] inayohusu wanawake kusaidiana

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2258

kwa mapishi. Tena kuna akdi [mikaha] msikitini au nyumbani. *Kisha kuibia au kuingia ndani kimyakimya au kwa watu wote kujua. Kisha kuna sherehe ya arusi kujibu, bi arusi anapohongera* (mlazo ni msisitizo wetu). Mradi arusi huwa mzigo mkubwa kwa wanaooa na wanaoolewa, na kwa kweli hakuna anayeikabili arusi hii peke yake kwa hali na mali…. Kubwa zaidi ni kwamba arusi lazima ichangamke ama kwa maulidi au kwa ngoma kutegemea itikadi za watu kidini na kimila….

Makala haya yaṭaelezeya asili ya neno "hongera" kupitiya makamusi ṭajika ya sasa na kale ya kiSwahili. Makala haya hayaṭoangaziya mabaḍiliko ya kiḍikroniya katika matumiyaji ya neno hili bali yaṭaakisi zama za matumiyaji yake minṭarafu ya watumiyaji wake wa kiSwahili Asiliya (SA) na kiSwahili Sanifu (SS) kama inavowasilišwa katika makamusi ya SS. K̇a kutumiya makamusi ni k̇a uwaminifu kuwa ni marejelezi ťika yaliyohifaďi maneno mengi ya luğa. Ďana 'kileo' na 'kisasa' ziṭatumika k̇a mpišano k̇a maana ya wakaṭi huu wa karne ya Iširini na Moja. Makala haya yaṭapeṇḍekeza k̇amba kuyapanuwa maana ya maneno ni katika sifa mojawapo za mabaḍiliko yanayokumba luğa zozoṭʰe ulim̓enguni lakini ṭahaďari zičukuliwe na wanaleksikografiya wanapotengeza makamusi. K̇a minṭarafu ya makala haya neno "hongera" lina asili ṭafauṭi na linavoelezwa makamusini leo na utumiyaji wake unaanika učafu k̇a sababu ya uṭafiṭi wa kina na mpana haukufanyiwa watumiyaji asiliya wa luğa hii ya kiSwahili. Maṭegemezi yetu yaṭaegemeya Naďariya ya Usemezano ya Mikhail Bakhtin (1981) inayošikiliya kuwa maana ya maneno haiyangaliliwi makamusini ṭu k̇a sababu luğa imo katika masemezano na jumuiya nzima ya mukṭaďa wa utumiyaji wake. Kuna vigezo va kihisṭoriya, kiusuli, kiuṭamaḍuni, kimukṭaďa, ainaṭi za luğa, na haṭa niya ya msemaji, hivo, kupata maana halisi lazima maana katika luğa iyangaliwe kupitiya vigezo hivi na venginevo ili kupatikane maana *haswa* ya neno. Fasiri ya ungonočoro au ungonografiya katika makala haya ni hali ya msisimko unawoṭokana na matumiyaji ya luğa au išara na alama zinazopelekeya kufikiri vitenro va ngono.

MBINU ZA UṬAFIṬI

Kama tulivoṭahaďariša kimbele kuhusu mauďuwi ya makala haya yanayohusu ungončoro au ungonografiya basi na mbinu za uṭafiṭi wake zina haja ya kuzipa ufafanuzi. Makala haya yaṭaťibitiša huko mbele kuwa hongera ni neno m̓iko k̇a waSwahili basi upokezi wa mṭafiṭi k̇a wasailiwa ulikuwa na vizingiti si haba. K̇anza, kuṭopata nafasi ya kumuhoji Profesa T.S.Y Sengo kuṭokana na masafa ya kumfikiya na upeyo wa uṭafiṭi wetu, tumetumiya kidahizo kama ušahiḍi hafifu lakini wenye mazingaṭiwa ili kutupa mšawaša wa kufanya uṭafiṭi wa kina. Pili, wasailiwa wanawake 3 kati ya 5 tulowaomba kuhojiwa walikataa kuulizwa kuhusu masiyala ya kingono. K̇a sababu aulizaye ni m̓anamume ṭena ajinabi halafu aṭaka kujuwa mambo ambayo, kiwawo, ni ya siri kʰuu na ya "kukosa aḍabu" na hili lačangiya ṭarakibu yetu k̇amba maneno m̓iko hayazungumzwi ni yoyoṭʰe popoṭʰe. Tatizo hili tulilitatuwa k̇a kumpata mtʰu-mzima ṭena m̓anamke—mama mSwahili na wa SA—wa miyaka zaiḍi ya 70 na ni m̓alimu mṭegemewa wa wasičana kuhusu mambo ya uwanauke katika jamii yake. M̓enyewe hujiita mtʰu-mzima na wala si kungwi au somo kama aitʰavo k̇engineko. Kuṭokana na msailiwa kumfahamu mṭafiṭi na kum̓apiya kuwa ni k̇a sababu ya elimu na haṭofanya hiyana ya kupotosha, nriyo alikubali kumfunza kitʰu mṭafiṭi katika maswali alouliza. Data tulokusanya k̇a msailiwa huyu (mtʰu-mzima) imeṭošeleza lengo la uṭafiṭi wetu k̇a kuwa aliyetufafanuliya masiyala haya ni m̓eledi na asemalo lina ťika. Pili, data ya kimsingi tuliikusanya k̇a mahojiyano na wasailiwa k̇a maswali yasomuunro kuhusu neno hongera na piya mafafanuzi yake ya kiuṭamaḍuni. Data tulopata k̇a wasailiwa wanaume na wanawake wa miyaka ya 55 k̇enra čini ilikuwa na tašwiši k̇a mḍangano wa majibu—hakuna kauli moja katika majibu. Nriposana tukaamuwa k̇itiya nguvu k̇a kutalii maaṇḍiko yaliyoko. Data ya kiupili tuliikusanya k̇a kupitiya maaṇḍiko ya waṭaalamu walofanya uṭafiṭi k̇enye mauďuwi haya na ilitusaiḍiya kučanganuwa maana zawo za

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2258

neno hongera tukiwa na uwaminifu k̇amba mlemeyo wa wasailiwa uṭapunguwa, uhakikišaji wa tuloyapata nyanjani yanafungamana, na mjaḍala wetu kuhusu neno hili una mašiko.

MAṬOKEYO

Hongera litumikavo kisasa

Katika upekuzi tuloufanya wakaṭi wa uṭafiṭi wa makala haya, tulitizama moja k̇a moja k̇enye makamusi k̇a sababu nriyo marejelezi ya upesi na aminifu. *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2016) (*KKK*) imefafanuwa hivi:

- **Hongera!** (kihisishi) tamko linalotumika wakati wa kumpa mtu pongezi baada ya kupata mafanikio fulani; heko.
- **Hongera** (nomino) neno la pongezi kwa kujikwamua kutoka kwa hali ngumu aghalabu ya kiuchumi na kupata mafanikio.

Mayelezo yoṭʰe mawili yanayegemeya maana mamoja k̇amba "hongera" ni "ku-pongeza" mtʰu k̇a hali ya mafanikiyo aliyoyapata. Ni kihisiši k̇a sababu linaṭowa hisi zilizomo nrani ya msemaji. Ni muhimu tujuwe k̇amba katika makamusi ya kileo (2010 na k̇enreleya) hongera limekuwa kidahizo kamili au tuseme ni neno kamili lenye kujisimamiya bila ya kuṭokana na neno jengine. Kulingana na ṭafsili hii hongera ni kupongeza na hutumika, si k̇a mawaṇḍa ya kufaulu kiučumi ṭu, bali haṭa kufaulu k̇engineko kama miṭihanini, mašinranoni, mavunoni na kaďalika.

Aiďan, tuliwauliza maswahibu marika zetu kuhusu maana ya neno hili "hongera" ili k̇aminiša kuwa nrivo haswa matumiyaji kileo. Kama huyo profesa k̇enye kidahizo ča RISSEA, maswahibu zetu nawo walijibu hivohivo kuwa hongera linamaaniša "kumpongeza mtʰu". Nasi tulikuwa na fikira hizohizo kama maswahibu zetu kabla ya tukiyo la RISSEA na kauli ya Profesa Sengo. Yaonekana fikira za maswahibu zetu, na mimi awali, ziliyaťiriwa ni mafafanuzi ya makamusi ya kileo na piya mazoweya ya kutumika hivo katika miji ya k̇etu huku uSwahilini hivi sasa kuṭokana na kufunzwa hivo, pengine mašuleni. Tuṭakuja k̇eleza baaḍaye, sivo kama watʰu wazima waliyotuziḍi kiumri, kina maprofesa Sengo na Khamis (SAM) na Bi Maryam Muhammaḍ "Nyanya Mkali" (k̇enreleya tuṭaṁita k̇a lakabu yake aipeṇḍayo ṁenyewe msailiwa wetu) wanavolitumiya neno hilo. Wazee hawa tunawowarejeleya hapa wana umri zaiḍi ya miyaka 70.

Hongera litumikavo awali

Upekuzi wetu ulitupeleka k̇enye makamusi ya kaḍimu tulopata kuyaangaliya: la L. Krapf (1882) na la C. Sacleux (1891/1939). Namnukuu Krapf kuhusu ufafanuzi wa hongera:

- **Hongera** (kitenzi) to wash the circumcised part in the sea [kuoša sehemu iliyoṭahiriwa baharini (TY)]. Watoto kwa siku ya sabaa tangu wametahiriwa waenenda pwani kuosha vidonda maji ya bahari. This is called ku-hongera [Hii yaiṫa kuhongera (TY)]. Watoto waliotahiriwa leo wamekwenda hongerwa or [au] kuoshwa maji ya bahari. On the sixth day the wounḍ is wrapped up in a piece of cotton soaked in oil, to prevent the urine affecting the wound [Katika siku ya siṭa lile jaraha (la kuṭahiriwa) hufungwa na kiṭambaa ča pʰamba kilorowešwa k̇enye mafuta ili kukinga mkojo usiďuru kidonra (TY)].

Sacleux naye anafafanua hongera k̇a maana mbili:

- a) Hongea, hongera, hongela ni maneno [paradimu] yanayotokana na neno la asili kwenye kidahizo "honga" (kitenzi) ambalo lilikopwa kutoka kiNyamwezi na kuingiya kiMrima [moja ya lahaja za SA kusini] kwa maana ya ada ya ruhusa ya kupita nchi fulani. Piya humaanisha kupata fadhila kutoka kwa mtu kwa kumpa kitu ili akupendelee kukipata kitu hicho.

  b) Anaenreleya kufafanuwa kuwa: hongera (kihisishi) ni neno aambiwalo mtu baada ya kuokoka na maafa fulani kwa mfano: kujifungua salama, kutahiriwa salama, kupona kutokana na ugonjwa, au kutoka safarini.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2258

- Hongerani! Kwa kiGunya (wenyewe hawapeṇḍi k̇iṫa hivo) humaaniša Shime!

Madan (1903, uk. 101) k̇enye kamusi lake analiweka neno hongera/hongela/hongea kama paradimu za "honga" (kitenzi) yenye maana ya kupata kitʰu kwa mapeṇḍeleo. Walakini yeye piya analiṭaja hili la k̇amba hongera/hongela ni awamu katika uponaji baaḍa ya kuṭahiri. Anayeleza piya ni ṭamko aambiwalo mtʰu kiṭamaťali k̇a mapongezi akisalimika na mikasa au akiṭoka safari, kujifunguwa salama. Lakini ṁišoni akaweka ṭanbihi kuhusu maana za maneno hayo k̇amba, "hayatumiki sana Zanzibar ağalabu ni matumiyaji na fikira za kuṭoka Bara [Ṭanganyika] na k̇amba turejelee "*For bribing*: rushwa, mlungula, kijiri, upenyezi *and for congratulations*: salimu, pukusa, -pa mkono, tunza, fichua."

Kuṭokana na mafafanuzi ya makamusi hayo tuloṭaja tunakuta k̇amba awali "hongera":

- Ni mnyumbuliko wa kitenzi "honga" lililokoṗa kuṭoka luğa nyengine ya kiBantu (kiNyamwezi) lenye maana ya 'rušwa'. Neno la asili la "hongo" katika SA ni "Chichiri" (Sacleux; Maḍan; Taylor, uk. 113; na TUKI).

- Ikapelekeya kupatikana hongea, hongela, hongera, hongeza, yaliyopata maana mpya ya kumpa mtʰu nguvu baaḍa ya mikasa kumfika.

- Piya humaaniša kušajiiša/kuhimiza kupambana na šiḍa iliyoko, k̇a mfano, katika neno "Šime".

- Ni šerehe au ni kitenro ča mfanyiko wa kuwaoša waliyoṭahiriwa huku uSwahilini wakaṭi wa kupaša ṭohara vijana wa kiyume.

Imeďihirika k̇amba neno "hongera" maana yake imebaḍilika k̇enye makamusi ya awali na ya kisasa. Kisarufi, lilikuwa paradimu ya kitenzi na sasa ni nomino na ṭangu awali na sasa ni kihisiši. Isipokuwa ṭafauṭi inakuja katika maana wakaṭi wa matumiyaji. Kisasa latumika k̇a maana ya "kupongeza" ṭu lakini huko nyuma lilimaaniša "pʰole, vumiliya, farijika". Ṫasema hivi k̇a sababu matumiyaji ya kihisiši čenye kumpa mtʰu ṁenye kufik̇a ni mikasa au maafa huku uSwahilini ni kuṁambiya, Pʰole! ima k̇a ugonjwa (ṭohara piya ni kuuguza kidonra), safari, kazi. K̇a mfano, *KKK* na Sacleux yameeleza "Pole!" (kihisiši) kuwa ni: a) tamko linalotolewa kwa mtu aliyepatwa na jambo baya kumliwaza; b) tamko analopewa mtu aliyechoka au anayefanya kazi ngumu, kwa mfano, pole kwa kazi Bwana Hassan. K̇a hivo, tukiyangaliya mayelezo ya "hongera" k̇enye makamusi ya awali (Sacleux na Madan) tuṭaona yamepotoka k̇a kutumiya "hongera" baḍala ya "pole" kama mafafanuzi yawo yanavolekeza ya misemo ya kinahau halisi inayotumiwa na waSwahili wenyewe wenye kutumiya SA. Makamusi ya *KKK* na hirimu zawo nayo yalikanganyika katika hilo na kučukuliya kuwa ni "kupongeza". Nasi ṫayauliza makamusi, hivi leo, mtʰu anapoṭoka au yumo ugonjwani, au safarini, au kazini anapawa pongezi au pʰole?"

Katika makamusi ya awali (Sacleux na Madan) neno "pongezi" k̇a maana ya kumpa mtʰu ṭahaniya k̇a ufanisi katika jambo limo; k̇a Krapf halimo. Sacleux anaeleza, "Pongezi kiMrima linamaaniša ṭamko analopawa mtʰu baaḍa ya kuṭoka safari au kujifunguwa salama anaambiwa "Pongezi!" naye anajibu "nimekwisha hongera", au "nimepona". Lakini Madan anaṭanbihiša kuwa si ağalabu kutumika Zanzibar, alipokuwako k̇a siku nyingi. Hili la kutumika uSwahilini ni muhimu sana k̇a sababu nrilo linaloṭafauṭiša maana ya halisi kupitiya watumiyaji wenye SA na utumiyaji wa mkopo uliyoingizwa katika SA. Bišop Steere (1919, uk. 172) katika oroďa yake ya ṭafsiri ya maneno muhimu anaṭafsiri "*congratulations*" k̇a "shangilia" na wala si "hongera" au "pongezi" kama tunavofasiri sisi kisiku hizi. Katika kazi hii ya Steere, ambayo ilitegemewa sana miyaka ya usanifišaji wa kiSwahili, na haṭa ya W. E. Ṭaylor (1891) neno "hongera" halipatikani kabisa. Mbali ya "šangiliya" waSwahili wanalo neno "Hariyo/Horiya!" (Sacleux) au "Howe!" W.E Ṭaylor (1891) katika meťali 'Howe ṇḍa ṁenye kufuma, wewe una howe gani?' ambalo hutumika wakaṭi wa ufanisi wa jahazi kuwonekana upeoni au kupata kiwiṇḍo mṭawaliya.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Kuṭokana na mafafanuzi ya neno kama neno, "hongera" na "pongezi" kupitiya maaṇḍiko yaliyopo ya zamani zaiḍi kuhusu SA – ya Krapf, Sacleux, Steere, Maḍan na Taylor tuṭaona kwamba maneno haya ni ya mkopo na ɗana zinazowasilišwa k̇azo uSwahilini zina visawe vake vinayosimamiya ɗana hizo, kama "pʰole" (nriposana akajibu "nimepona") na "šangiliya" mṭawaliya. Ya k̇amba ṭangu awali "hongera" haikumaaniša "pongezi" (*congratulation*) k̇a minṭarafu ya matumiyaji yake kale na sasa yenye maana ya fariji, tuliza, au liwaza kuṭokana na matukiyo mabaya yaliyompata mtʰu. Ya k̇amba "hongera" ni šerehe katika ṭohara ya vijana k̇a minṭarafu ya Krapf aliyekaa sana huku Mambasa kuliko na mojawapo ya SA. Hili la kuwa ni šerehe nrilo liṭakalotušuğuliša katika sehemu ya pili ya kulitatuwa neno "hongera" kulingana na mukṭaɗa wa uṭamaḍuni wa waSwahili ambawo hujiyeleza kupitiya luğa yawo SA.

Hongera kwenye mukṭaɗa wa uṭamaḍuni

Bakhtin (1981) ana msimamo k̇amba luğa imo katika masemezano baina ya luğa na luğa, ɗana na ɗana, luğa na mazingira inamotumiwa, yaani luğa haiko pekee bali imo katika jumuiya nzima ya mawasiliyano. Nriposana Bakhtin akašikiliya kuwa kipašiyo kikʰuu katika mawasiliyano si neno bali kauli. K̇a sababu, k̇angaliya maana ya neno kamusini ni kupata maana ya juujuu lakini kupata maana ya halisi hubiḍi izingatiwe vigezo kama usuli na mapisi ya neno, mukṭaɗa wa matumiyaji katika jamii, sajili itumikayo, aina za luğa zilizomo nrani ya luğa hiyohiyo moja: kifasihi, kiṭaalamu, kikawaiḍa, na zaiḍi, niya ya msemaji ikiwa yaweza k̇akisika. Huu nriyo msingi wa kinaɗariya tunawouṭegemeya sisi katika kusema kuwa maana ya "hongera" k̇enye makamusi ilikuwa haiṭoši tukirejeleya matumiyaji katika jamii ya waSwahili na uṭamaḍuni wawo. Ṫelewe waSwahili (watʰu) na uSwahili (uṭamaḍuni) upo na warejelewa hivo katika masiyala ya kiluğa na uṭamaḍuni haṭa katika maaṇḍiko ya kisasa yenye kušereheša SS, mfano *KKK* linapofafanuwa "harusi" na maana ya 'harusi kujibu'. Sehemu hii iṭajaḍili maana ya "hongera" katika mawaṇḍa mawili ambayo yanačangiyana kupa maana halisi kulingana na SA: kiṭamaḍuni na kifasihi. Fasihi ni sanaa ya luğa inayočota mawazo yake kuṭokana na jamii husika. Na uṭamaḍuni, k̇a učače, ni *namna* jamii inavojiyeleza katika miyonroko yake ya kimaiša. Luğa, ikiwamo kama kipengele kimojawapo ča uṭamaḍuni, ni "ḍiriša" la kuwoneya yaliyomo nrani ya jamii hiyo.

Hongera ni awamu katika šerehe

Tunaposoma Mbaabu (1985) tuṭaona kuwa waSwahili walikuwa na uṭamaḍuni wa ṭohara ṭangu azali na waliyuwenreleza kila msimu wake unapowaḍiya. Ilikuwa ḍasṭuri nzima ya ṭohara ikifanywa katika sehemu (zikiiṫa kumbi) mbali na mjini ili kuhifaɗi kunga/siri za mila hiyo. Humo vijana hutiwa unyagoni k̇a wasičana na janroni k̇a wavulana/wačʰuvuli. Makungwi manyakanga huwapa vijana hawa mafunzo ya utʰu-zima ili waweze k̇iši kama wanavopaswa katika jamii. Wavulana na wasičana hufunzwa mengi ya kuṭekeleza majukumu yawo waṭakapokuwa mume na mke nyumbani haṭa waṭakapoonana kiṁili. Lakini yoṭʰe haya hufanywa k̇a siri kʰuu na wanafunzi woṭʰe hulišwa viyapo va kuṭosema loloṭʰe kuhusu yaliyoseṁa na kutenrwa humo (Strobel, 1979 uk. 209).

Wačʰuvuli

Kama tulivok̇išaeleza awali k̇amba "hongera" ni awamu katika šerehe ya ṭohara k̇a upanre wa wavulana (Krapf, 1882). Ni wakaṭi (siku ya sabaa baaḍa ya kuṭahiriwa) wa kupelek̇a wavulana kuošwa k̇a maji ya bahari viḍonra vawo baaḍa ya kukatwa vigozi k̇enye mb8ro zawo. Haya hufanzwa huko huko msituni, zamani Mgongeni, Kisauni, Mambasa (Nyanya Mkali mazungumzo naye Ng'ombeni, K̇ale, 01/08/2024). Čini ya usimamizi angalifu, ngariba anawauguza vijana hawa mpaka wanapopowa na k̇ačiwa kuṭoka kumbini kama watʰu wazima. Hili la kukaṫa kigozi hičo ni tenro zitʰo na la kuwogofya sana haṭa huwafanya wavulana wengine wasihuɗuriye wača kuhiṭari kukaṫa huko janroni; siku hizi wengi hukaṫa kigozi sipitalini (Walibora, 2016). Ama kuhusu wasičana waSwahili, hakukuwa na kupaša ṭohara k̇awo bali wawo hupelek̇a k̇a

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2258

Nyakanga/Kungwi (maneno yaliyokoṗa kuṭoka Tanzania Bara), au somo (huku Ṗani kaskazini) kufunzwa mambo ya uwanauke katika nyumba zawo (Strobel 1979, kur. 196 & 200)

Mahavule

Kama wavulana wačʰuvuli, na k̇a wasiČana/mahavule, "hongera" ni awamu katika šerehe lakini si ya ṭohara bali katika harusi/arusi. Katika ḍonroo la *Mhanga Nafsi Yangu* tulilonukuu awali, tuṭaona ni sehemu/awamu ipi ambapo hongera limetumika. SAM anasema hivi:

Tena kuna akdi [mikaha] msikitini au nyumbani. *Kisha kuibia au kuingia ndani kimyakimya au kwa watu wote kujua. Kisha kuna sherehe ya arusi kujibu, bi arusi anapohongera* (mlazo ni msisitizo wetu) (SAM, 2015, uk. 150).

Baaḍa ya SAM kuraṭibiša kimuwala, haṭuwa moja haḍi nyengine ya mfanyiko mzima wa nrowa—ṭangu kupeṇḍa k̇a mačo haḍi kukutaniša wapenzi wawili rasmi—anafikiya k̇enye mikaha ambayo ni šerehe ya kufungwa k̇a nrowa baina ya maharusi msikitini au nyumbani, kiša k̇ingiya nrani yaani ɓanaharusi kukutana na biharusi kiṁili. Kabla ya awamu ya k̇ingiya nrani k̇anza kuna šerehe SAM aliğafilika nazo: ya kufunguwa mlango—na kabla yake kufunga mlango—ambapo ɓanaharusi huṭozwa aḍa fulani mlangoni haswa na mašemegize mume ambawo "walimlinra" mkewe asiwe akiṭoka nje ila mpaka na wawo; na ya kuṭowa mkono ambapo ɓanaharusi hukaribišwa nrani k̇a kina biharusi kuja kuṁamkuwa mkewe na kumpa mkono wa furaha k̇a woṭʰe wawili kukubali kuwa mke na mume kišariya na kumpa zawaḍi mkononi bila watʰu kujuwa ni nini aličozawiḍiwa. Maharusi hulišwa vakula vičače huku nrani, na waliyoko nje, marafikize ɓanaharusi, hupawa katika kombe la ɓanaharusi—čakula kiličoanraliwa mahususi k̇a waliyoaṇḍamana na ɓanaharusi (kuṭoka maaṇḍiko yangu nyanjani na mazungumzo na Nyanya Mkali 01/08/2024).

Kuhongera na harusi kujibu

Kama ilivo ḍasṭuri uSwahilini, ɓana hwingiya nyumbani k̇a kina bibi au yawezekana k̇ingiya nyumbani k̇a mume kama ilivo kisiku hizi. Watʰu muhimu katika šuğuli hii ya k̇ingiya nrani ni: mtʰu-mzima (kama alivoṭaka kuṁita Nyanya Mkali na wala siyo kungwi k̇a sababu hawak̇iṫa hivo huko Mambasa) ambaye nriye aliyemfunza huyu biharusi mambo ya unyumba (Strobel, 1979, uk. 12) na šangazile mume. Wakaṭi wa k̇ingiya nrani ukifika, ɓanaharusi huṭolewa nje k̇enye čumba ča maharusi akaṭayarišwa čumba čengine k̇a šuğuli hii muhimu. Bibiharusi naye hujiliwa ni mtʰu-mzima wake na šangazile mume kumuuliza kama "yuko sawa" yaani ni bikira. Jawabu ya bibiharusi ikiwa sawa basi hwelezwa na mtʰu-mzima wake atuliye wala asibabaike; akaye tuli aṁače yule ɓana aṭakapokuja "kušika nyumba" afanye kitenro ča kuvunja kizinra ča ṁanaṁali huyo. KiMambasa na k̇elekeya kaskazini lile tenro la kuṁingiliya mkewe k̇a mara ya k̇anza hwiṫa "kufanya harusi". Yumkini piya "harusi", k̇a mukṭaďa wa kuhongera, iličukuliwa kuṭoka wavulana wanapopašwa ṭohara ambapo kiSwahili hwiṫa "harusi" (Timammy, 2002, uk. 36). Sawiya katika awamu hii bibiharusi piya aṭakaṫa kizinra na mumewe hivo kuwafiki k̇iṫa harusi. Nahau hii au maana hii ya harusi haikuṭajwa na walimu Mohamed & Mohamed (2002) wala na makamusi ya kileo.

Mtʰu-mzima anamšauri ṁari wake ajizuwiye astahimili maumivu hayo. Wanaume wanawojiweza "kisawasawa", čembelečo Nyanya Mkali, huwa ni kazi ya mara moja. Katika šuğuli hii bibiharusi anapata maumivu, ya kisaikolojiya na ya kiṁili, anapoingiliwa k̇a mara ya k̇anza (Ferguson, 2019). Si hayo tu, na watu waṇkaa nje wasikiza viliyo vake waongojeya jawabu (W.H Ingrams akinukuliwa ni Strobel, 1979, uk. 12). Akimaliza kumbikiri mkewe basi mume hugonga mlango na huṭolewa k̇enra kuwoga; na mtʰu-mzima na šangazile ɓanaharusi huwa wa k̇anza k̇ingiya nrani na k̇angaliya kisarawaṇḍa, kiṭambara čeupe kinačotanrik̇a k̇enye firaši mahususi k̇a jukumu la kutonewa ḍamu ya kubikiriwa mke (Strobel, 1979, uk.12).

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Wakišaona watʰu wawili hawa hwiṫa šangazile mke na nyanyake mke waje wašuhuḍiye na wawo ḍamu hiyo ya ubikira na hapo harusi imejibu ḳamba mambo ni mazuri msičana anakuwa mke wa ɓana.

Furaha ya ɓanaharusi kumpata mkewe bikira yeye huṭowa jazuwa (zawaḍi), ima pete, pesa au zawadi yoyoṭʰe iṭakayomfurahiša mkewe kwa kuhifaďi ubikira wake haḍi siku hiyo. La sivo, harusi haikujibu vizuri, mke anaačika hapohapo ḳa waSwahili kulingana na Nyanya Mkali. Awamu hii nriyo kuhongera na nrivo alivoniyeleza Nyanya Mkali (mazungumzo naye Ng'ombeni, Ḳale 01/08/2024) piya yameṭajwa ni Middleton (1996) na kuťibiṭiša maneno ya SAM katika donroo lake tulilonukuu huko nyuma.

Huku nje wakaṭi wa šuğuli ya kufanya harusi au kušika nyumba inapoenreleya, wanawake waliyoolewa wanaimba nyimbo ambazo zamšajiiša ṁari-mke katika kulikabili tukiyo hilo la kubikiriwa. Wanaimba nyimbo maarufu maharusini, lakini čembelečo Krapf (1882, uk. 261), Strobel (1979, uk. 207-8) ťamma na Nyanya Mkali watʰu hawaelewi ṭena maana ya maneno na nyimbo ziimɓazo hivo hujiimbiya bila kujuwa wapi hwimɓa nyimbo ipi. Kulingana na (Ali, 2014), aliyegawa awamu hizi za šerehe za arusi 'kimikṭaďa', anaeleza kuwa kila mukṭaďa (kisisi awamu ḳenye šerehe ya harusi) una nyimbo unazoaṇḍamana nawo. Ḳa mfano, wakaṭi ɓanaharusi anapokuja kuṭowa mkono anakuja na wafuwasi wake huku inaimɓa nyimbo maarufu huku Mambasa:

> Mamaye harusi ṇḍoo kaole
>
> Kaole mgeni kangiya
>
> Mgeni kongo
>
> Hayayee kaole mgeni kangiya

Kinaťari mamake harusi anaiṫa akatizame mgeni (ɓanaharusi) amefika na akaribišwe.

> Wakaṭi ɓanaharusi ameingiya nrani kufanya harusi hwimɓa nyimbo ya:
>
> Leo ni leo ooo x2
>
> Tuṭauwona mpambano
>
> Kweli si urongo

Katika kumšajiiša ṁari-mke wakaṭi wa kuhongera na kupata ṭaabu anaimbiwa:

> Hongera mwanangu hongera,
>
> Nami nihongere wee hongera
>
> Mama uṭungu mama uṭungu
>
> Nyamala mwanangu hoyee
>
> Nyamala mwanangu tumbo la uḍere
>
> laniuma mno we hoyee
>
> laniuma mno we hoyee
>
> Eee laniuma mno wee,
>
> Nipani pole wenzangu
>
> Oyee laniuma mno weee hoyee.

Imečukuliwa kuṭoka ḳa Ali (2014, uk. 185) na Matona (2020) lakini kuna mabaḍiliko haṭa ḳa Timammy (2002, uk. 233-4) kuwafiki alivonisahihiša Nyanya Mkali wa Mambasa na sasa Ng'ombeni, Ḳale. Yaonekana ni ṭafauṭi za kimaṭamši hivo kuwa aina ya toleo lengine: kama wasemavo kila nyimbo ina nṭʰa sabaa.

Na wakaṭi wa mukṭaďa wa harusi išajibu na kisarawaṇḍa kišakunjwa na kuweḳa ḳenye kisahani na kufuniḳa nyimbo nyengine inaimɓa:

> Mamaye mume na mamaye mke
>
> Ṇḍooni muwone kibereko

Krapf amikiita "ubeleko" kuwa ni zawaḍi apawayo mameharusi wakaṭi wa harusi.

Tumewona kuṭokana na mafafanuzi hayo ḳamba kila haṭuwa ina mayelekezo yake na hušerehešwa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2258

k̇a nyimbo zake ili kutiya laďa šuğuli lakini piya kusema kitʰu kuhusu šuğuli hiyo. K̇anza kabisa ni k̇amba nyimbo zoṭʰe za harusini uSwahilini hwimḃa ni wanawake watupu ingawa wapigaji ngoma, mara nyengine, ni wanaume. Pili, upigaji ngoma huwo na uwimbaji hufanywa, ima nyumbani k̇a maharusi woṭʰe wawili au kisiku hizi k̇enye kumbi zinazokubaliya wanawake watupu, k̇enye kawaṇḍa maalumu lililozungušwa bigili linaloziba watʰu (haswa wanaume) wasipate kuwona nrani. Tatu, kuna muwala muhakamu wa mawasilišo ya nyimbo kulingana na awamu ya šerehe. Kuṭokana na uwangalizi wetu, ni wazi kuwa "hongera", kisasa, limehifaďika katika nyimbo inayohusiyana na k̇ingiya nrani mume na kufanya harusi k̇a maana ya kumbikiri ṁari-mke. Mikaha yamfungiša kuwa mke lakini anabaki ṁari haḍi siku na saa ya kubikiriwa.

Makala haya yanamsahihiša Ali (2014) k̇a kuuweka wimbo wa "hongera mwanangu hongera" katika mukṭaďa wa *baaḍa* ya harusi kujibu (uk. 65, 185, & 195). Yamkini Ali aliğafilišwa ni maana iliyoko haďirani kuwa "hongera" ni "kupongeza" nripo wimbo huu unaleṫa "baaḍa ya" bibiharusi kubikiriwa na kupatikana salama, kuwa ni bikira (kur. 4 & 21). Katika mayelezo yake anayeleza kuwa ni, "[a] kumpongeza bibi harusi anapokutwa bikira siku ya harusi…[b] inamaanisha heshima … anaipata mama mzazi. Kwa malezi bora…. (Ali, 2014, uk. 154). Tumesema Ali "alighafilishwa" lakini piya ṫaweza kusema alijikanganya k̇a kutumiya hongera k̇a maana mbili: a) ni ṭamko la "kumpongeza" biharusi k̇a kupatikana bikira; na b) ni *kitenro* ča k̇ingiya nrani ḃanaharusi kufanya harusi. Mkanganyiko wa maana k̇amba hongera ni kitenro ča au ni wakaṭi wa kuṁingiliya biharusi unapatikana anaposema "Yaani mwari amehongera" (katika mayelezo ya Picha 1 uk. 21); "[Sahani] hupitishwa mbele ya hadhira baada ya bibi harusi kuhongera" (Maelezo ya Istilahi ya "Sahani ya somo" uk. 37); na "miktadha ni kama vile…kumchukua bibi harusi, kupokea masanduku ya bibi harusi, bibi harusi anapohongera na siku ya kupamba" (Upeo na Mipaka, uk. 33). K̇a maoni yetu, k̇enye wimbo huwo wa "hongera mwanangu" kumetumika maneno yanayolekeza katika msongonyeko wa mambo magumu yampatayo ṁari wakaṭi wa tenro hilo la kukutana kiṁili na "ṁanamume" mara ya k̇anza. Wimbo huwo una maneno kama: hongera, ṁanangu, nami nihongere, uṭungu/učungu, nyamala/nyamaa, tumbo la uḍere/ugere/ukere, laniuma mno. Ṁišoni mama anasema "nipani pole". Maneno hayo yoṭʰe yanajenga ile ṭaswira na manďari ya maumivu yaliyomo katika kubikiriwa. Ṁana au ṁari anaambiwa na mamaye avumiliye kama yeye (mama) anahisi anavoumiya ṁanawe k̇a sababu tumbo la uḍere/undere/ukere (la kukerekeṭa/kukera) lamuuma sana mama. Nriposana ṁišoni ṁa wimbo anaomba apawe pʰole. Hivo basi, Ali anawafikiyana na maana yetu k̇amba hongera ni kile kitenro ča ngono siku ya kufanya harusi tukitiliya maanani ufafanuzi wake wa isṭilahi na mayelezo ya pičani.

Kama tulivotanguliya k̇eleza awali kuwa "hongera" lina maana ya "kumpa mtʰu pʰole" kuṭokana na maafa yanayompata na tukawona namna ṁari ṁanagenzi wa mambo haya anavohisi siku ya ṁanzo katika mambo haya, basi yawafiki zaiḍi kuwa "hongera" ni ṭamko, ima kihisiši ča "pʰole" au ni kile kitenro ča kufanya harusi ambačo ni kigumu na ṁari aomḃa asubiri k̇ačo. Mbona mama hakuliliya kupawa "pongezi" k̇a sababu ṁanawe amepatikana bikira? Učanganuzi kauli wa wimbo wenyewe k̇a kuratibiša uwiyano na ufungamanišo wa maneno uṭatupa ufunuwo na uwafiki wa maana yetu ya hongera kuliko itumikavo kamusini leo. Wimbo unaimḃa hivi:

Wimbo asiliya		Wimbo baḍali
Hongera mwanangu *hongera*	*pongezi* mwanangu *pongezi*	*pʰole* mwanangu *pʰole*
Nami ni*hongere* wee *hongera*	nami ni*pongeze pongezi*	nami ni*powe pʰole*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2258

K̇a kubaḍiliša neno hongera katika kifungu ča ṁanzo na kuwek̇a pʰole au pongezi katika mišororo ya vifungu va baaḍaye tuṭaona kiyučanganuzi kauli ni kauli zipi ambazo ziṭazališa unguliko la mama kusema /mama uchungu mama uchungu/ na ṁišoni kuwomba apawe pole. Ni wazi neno lenye kuwafiki katika mjarabu huwo ni pʰole au vumiliya kama tulivofafanuwa sisi na wala si pongezi kama imaanišavo kileo. Yowe la kušangiliya la pongezi! halizališi kauli ya „nipani pole" kama ilivodonrolewa k̇enye wimbo huwo awali huko nyuma.

Aiďan, ṭangu ṁanzo tumesema kuwa "hongera" katika maaṇḍiko ya kale lilikuwa kitenzi au kihisiši lakini sasa nriyo limebaḍilika na kuwa nomino, k̇a mfano katika *KKK*. Ikizingaṭiwa donroo la SAM "sherehe ya arusi kujibu, bi arusi anapohongera" tunafahamu kuwa "sherehe ya arusi kujibu" ni "kufanya tenro la nrowa" na k̇amba kišazi ča pili "bi arusi anapohongera" ni ufafanuzi wa kišazi kiličotanguliya ča hiyo arusi k̇afanyika nini nako ni kumbikiri ṁari-mke sawiya na ilivofafanuliwa katika *KKK* kuhusu "harusi kujibu", na sisi, "kufanya harusi". Seuze Profesa Sengo alipokataza, k̇a kukemeya, lisitumike neno hilo k̇a maana ya "pongezi". K̇a minṭarafu ya mafafanuzi yetu yawezekana hongera lilikuwa awali ni kuṭowa pʰole lakini k̇a waSwahili liličukuwa maana mpya na finyu yenye maana ya kufanya ngono k̇a kuwa neno lenyewe limehifaďika katika wimbo unawoimḃa mahususi wakaṭi wa k̇ingiya nrani ḃanaharusi.

Hongera kwenye mukṭaďa wa kifasihi

Kuzungumza k̇a mafumbo au k̇a siṭiyara ni katika ubingwa wa watumiyaji wa luğa yoyoṭʰe uliṁenguni. Na katika mambo yanayohusiyana na maneno ṁiko ya ḍaraja ya juu (k̇a mfano, ngono huku uSwahilini) basi haṭa ṭasfiḍa zake baḍo huwa za kimafumbo. K̇a mfano msemo "mṭaimbo kubomowa nyumba" k̇a maana ya "mb8o" au tenro la ngono (Charles & Ochieng, 2023). Iṭaṭaka umahiri wa kiyasi fulani wa luğa kujuwa maana ya maneno au nyimbo zinazoimḃa wakaṭi wa šerehe au k̇enye matambiko ya kijamii.

Šerehe ya aina yoyoṭʰe ina zamu maalumu ya kufanyika. Hivi nrivo donroo la SAM lilivosawiri šerehe ya harusi huko Motoni [uSwahilini] na k̇amba huwa na ṁanzo na ṁišo. Pili, šerehe ya harusi ya kiSwahili hušangiliwa zaiḍi ni wanawake kuliko wanaume. Tatu, kila jambo hufanywa na wanawake hawa pekeyawo pekeyawo, kama k̇a siri, ikawa wanaume hawakurubii mahali walipo wawo. Si bina basi mambo hayo ni ya kunga (siri) na waenrešaji wake Tanzania wakaiṫa makungwi—waliyofanywa kuwa wasiri (Strobel, 1979, uk. 11) na watʰu-wazima yaani mašangazi na manyanya nriyo wahusika wakuu. Katika mkusanyiko huu kuna luğa ya aina pekee ambayo haitumiki nje ya boma hilo la harusi. Luğa hii huwa ina maṭuši nrani yake yenye k̇eleza mambo mengine k̇a mafumbo magumu kufahamika "ḍakṭari aja tiya kidonra ḍawa" na mengine k̇a mafumbo mepesi kujulikana "ḃanaharusi aṭaka kiṭabu ačore" wakaṭi yuwaja kuṭowa mkono au kumčukuwa mkewe (Ali, 2014, uk.183). Au, k̇aweza kutukanwa waziwazi, k̇a mfano, nyimbo za "baburau ana marere", "sijauwona mpilipili", "mnazi wapanra watʰu wawili", "simba yoyoyo simba nakula nyama", au "kila siku kičočoroni leo kitanrani" (kuṭoka maaṇḍiko ya nyanjani). Kulingana na Strobel (1979) makungwi hufiča maana za nyimbo "nzitʰo" k̇a sababu kila kungwi ana hakimiliki juu ya ṭaaluma yake hivo hawapi yoṭʰe waṭakawo. Kulingana na Krapf ukurasa 261 makungwi hufiča maana za nyimbo hizo ili kuwafanya wari wawe wajinga milele wamtegemee kungwi ḍaima.

Tukitizama manďari mazima ya šerehe ya nrowa tuṭaona kuna išara na alama zinazotumika na zenye kusiṭiri maana ila mtizamaji awe na umakinifu wa kušikaniša moja na jengine apate kufungukiwa ni maana baṭini. Ḃanaharusi nriye anayepawa uzitʰo katika šerehe k̇a sababu mume nriye aowaye—mke huwolewa— čembelečo Nyanya Mkali, hawaowani uSwahilini. Mbali ya čeo piya anapawa na mamlaka juu ya mke na nyumba. Mume anaaširiwa k̇a mti (mtenre, mnazi), simba; na mke anapawa išara ya njiwa, koo, nyumba. Zoṭʰe hizo ni kumfanya mume awe haďi ya juu na mke ṁororo ṭena nyoofu čini. Kuna

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2258

alama za ḍakṭari, siṇḍano na jipu, kiṭabu na kalamu, mti, mči na kinu, (ma)čakača (majani makavu) na mpilipili na mauwa yake, na mkiya. Fasiri za nrani ziṭak̇ambiya išara na alama hizi zikiṭajwa katika manďari na mahali hapa harusini basi zinawakilišwa sehemu nyeṭi za maharusi.

Tukirejeleya ploti ya mume k̇ingiya nrani tuṭawona kila haṭuwa ina tenro lake ḍogo linaloaṇḍamana na nyimbo maalumu za bibiharusi akišapawa mkono, akišakula kombe la ḃanaharusi, akišatiwa čooni kwogeshwa, inapoṭaka kufanywa harusi, akišašikishwa nyumba, na furaha yake kupaṫa bikira. Wimbo wa “hongera ṁanangu”, tuliyonukuu awali, hwimḃa wakaṭi mahususi nawo ni wakaṭi wa kufanya harusi. Išara zinazotumika ni za: maumivu (k̇a woṭ^{h}e ṁari-mke na mamama zake), tumbo kuuma ṭena lauma sana, na mkerekeṭo huwo unawoṭokana na kusagika mačango. Maumivu haya yanaweza kuṭokana na mčečeto unawoṁingiya ṁari-mke k̇a sababu ya mara ya k̇anza kufanya tenro lile. Na k̇a mama, inaweza kuwa ni umit^{h}o wa ṁanawe anasikiya učungu lakini piya yaweza kuwa ana wasiwasi ṁanawe aṭapatikana bikira? Tukumbuke wanawokuja kumuuliza binṭi kama “yuko sawa” ni šangazile mume na mt^{h}u-mzima wake haṭa mama hajuwi ṁanawe alivo. Fauka ya hayo, sehemu iloṭeuliwa ya kuuma si kičwa – k̇a maumivu ya kisaikolojiya – bali ni tumbo sehemu ya čini katika ṁili wa binaḍamu penye mfuko wa uzazi. Hakukuṭajwa maumivu katika šerehe nzima ila katika ploti hii ya k̇ingiya nrani k̇a sababu yanaṭokana na kule kubikiri ṁari iliyo na učungu mkali kama ilivoelezwa na Ferguson (2019). Yamkini, katika kumfunuliya ṁari wawo maumivu haya ni katika kumšajiiša (Timammy, 2002, uk.110 hongera k̇a maana ya “shime” aliiṭafsiri *succeed*) kuwa ni ya kuvumiliwa k̇a sababu ni tenro la mara moja na, wawo na yeye biharusi, waṭapona.

Toni ya nyimbo zenyewe ni zenye midunro na ṁenro wa harakaharaka. Mfano ni huwo wimbo tulonukuu ya “leo ni leo” inaďihirika k̇imḃa k̇a sauṭi yenye kuweka hekaheka za vita au ngondo/k^{h}onro kuṭokeya. Ukija k̇a wimbo wa “hongera ṁanangu” huwanza k̇a mdunro wa kimasikiṭiko k̇a kutumiwa hongera (p^{h}ole), tumbo kuuma, učungu anawousikiya mama, na ṁišowe linapomziḍi unguliko hilo mama anaomba afarijiwe. Baaḍa ya beṭi hizi k̇iša hwanza toni ya juu ya kumuwasa mke kuhusu unyumba na nyumba yake k̇a umuhimu wake. Hufikiya kilele ča juu čenye sauṭi kali ya kušangiliya mti kukatika ka! au nyumba kubomoka ka! (Matona, 2020; Timammy, 2002, uk.245) k̇a sababu “kazi” imek̇isha au yamalizwa huko nrani.

Kuṭokana na mayelezo haya ni wazi kuwa mfanyiko mzima wa harusi umejaa šamrašamra lakini piya una mafumbo mengi ya “kukosa aḍabu”. Kulingana na Nyanya Mkali anafahamiša k̇amba učafu huu ni wa hapo harusini ṭu, k̇a wanawake ṭu, ṭena uwani. Labda manďari yenyewe yametengeza mahali pa kuzungumziwa ngono ṭu kwani nriyo mwisho wa šerehe mume anapomčukuwa mkewe; baaḍa ya hapo kila mmoja hufululiza k̇ake. Ikiša harusi aḍabu huruḍi na kila mmoja hučunga hešima ya ṁenzake. Nyanya Mkali aliniyeleza k̇amba hapeṇḍeleyi wafanyavo “makungwi” k̇a kuṭaja mambo ya siri “mačafu” k̇a uwazi mbele ya haďira (k̇enye iďaa za televisheni na rediyoni) isokuwa harusini. Yeye binafsi anapopiga goma la harusi (babake alikuwa, na yeye ni sogora wa wanawake) huṁambiya mnyakaji video afanye uhariri k̇a maneno mačafu aṭakayoyaṭowa wakaṭi huwo.

Bakhtin (1986) anasema kuwa maana ya neno haibakii hiyohiyo hubaḍilika kila siku kila wakaṭi kuṭokana na mivutano ya nrani k̇a nrani kuṭokana na kubaḍilika k̇a mazingira ya matumiyaji na nrivo ilivo haṭa katika mabaḍiliko ya kisemantiki katika mpito wa wakaṭi. Mayelezo ya aina hii yaṭawafiki katika maneno ya kawaiḍa, k̇a mfano neno “šabiki” miyaka ya ťamanini katika matumiyaji mapana lilimaaniša *substitute* (kama k̇enye kanranra) na leo ni mfuwasi wa uraibu wowoṭ^{h}e hususani burudanini. Ama k̇enye maneno yahifaďiyo uṭamaḍuni wa jamii, na hapa ni SA, iṭakuwaje yawe ṁiko ya daraja ya juu k̇a waSwahili halafu maana ya makamusini kileo iwe ni ṭafauṭi kabisa wača kuwa ni ṁiko? Pili, masiyala ya kuvunja haďi na hešima k̇a msimu maalumu yanapatikana katika šerehe ya

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2258

kimaharajani Ulaya, k̇a hivo, ni ule umaharajani nriyo unawohalališa “učafu”. Lakini maneno “mačafu” yatumiwayo k̇enye maharajani yana niya ya unenibezo k̇a kukejeli miyunro iliyowek̇a ni waṭawala katika jamii. Sasa tukičukuliya hivi k̇amba ni unenibezo, wanawoambiwa “hongera!” wakati wa kupongezwa k̇a kazi nzuri waloifanya wako ṭayari kukubali kuwa wanabezwa? Haiyumkiniki. Iṭoše basi, kuwa mwahali mutatu: kwenye masimulizi rasmi, kiṭamaḍuni, na kikawaiḍa neno “hongera” haliwafiki kutumiwa k̇a maana ya “pongezi” k̇a sababu linanasibišwa na ungonochoro uSwahilini, wekahazina wa kiSwahili.

HIṬIMIŠO

Imekuwa azma ya makala haya kuṭowa mafafanuzi mačače kuhusu neno “hongera” katika matumiyaji yake kisiku hizi. Data yetu tuliikusanya kuṭoka k̇a makamusi ya kiSwahili yenye ťika kiuwaminifu wake. Makamusi ya Krapf, Sacleux, Madan, TUKI na *KKK* yalirejelewa. Piya tulirejeleya wasailiwa wenye umri zaiḍi ya miyaka 70 tuliyowahi, k̇a muḍa mčače na upeyo mfupi tuliyokuwa nawo, kuwahoji na wawo kutufahamiša kit^{h}u katika maana mbalimbali za neno hili.

Uṭafiṭi wetu umegunruwa kuwa neno hili usuli wake ni la mkopo kuṭoka luğa umbule kiSwahili: kiNyamwezi kupitiya dadake kiMrima. Haswa lilikuwa na maana ya “p^{h}ole” apawayo mt^{h}u k̇a k̇aťirika na maafa. Walakini, yamkini wakaṭi fulani lilipoingiya uSwahilini lilimaaniša aina ya šerehe katika mfanyiko mzima wa upašaji ṭohara wavulana kama alivoeleza Krapf. Kuṭokana na maaṇḍiko ya waṭaalamu wengine kama SAM tumepata kujuwa hongera piya ni aina ya šerehe ya harusi ya kiSwahili lakini yenye kuhusiyana na ngono. Mayelezo haya piya yamekaririwa ni mt^{h}u-mzima Nyanya Mkali ṁenye ujuzi wa kuwaleya na kuwakuza mabanaṭi kuhusu unyumba na mambo ya majumbani. Yamkini lilipoingiya kiSwahilini lilipawa maana mpya ṭena ikafinywa na kubaki katika masiyala ya ngono ṭu. Nriposana k̇enye kidahizo tuličoṭaja profesa wa kiSwahili Sengo alikataza matumiyaji ya “hongera” k̇a maana ya “kupongeza”. Alhasili, naďariya tete yetu ya maana hupatikana k̇a k̇angaliya vigezo vingine kama: usuli, mapisi, uṭamaḍuni, sajili, na niya zaiḍi ya maana ya kikamusi imeťubuṭika; maana ya kikamusi katika mafafanuzi yetu imevunjwa na maana ya kiṭamaḍuni inayolifanya liwe neno ṁiko. Haṭimaye, lengo letu limeṭimilika, k̇amba “hongera” kutumika k̇a “pongezi” ni k̇anika ungono haďarani. Kuṭokana na mafafanuzi yetu k̇amba uṭafiṭi ufanywe haḍi k̇a watumiyaji Asiliya wa luğa hii; je, isṭilahi “msag8” k̇enye aina ya ploti tusemeje? Na je, haujafika basi wakaṭi wa Baraza la kiSwahili Kenya (BASWAKE) kuzawa na kusaiḍiya kuṭekeleza hayo juu ya k̇amba ruhusa kuunrwa k̇ake iṇšaṭolewa ni Serikali?

ŠUKURANI

Asanṭa k^{h}uu iṁenree Ṁalimu Maryam Muhammaḍ “Ṁanaimamu Nyanya Mkali”, Mngu atuwekee, alikuwako Kisauni na sasa Ng’ombeni, K̇ale na woṭ^{h}e walonisaiḍiya k̇a fikira kuweza k̇eleza mačače kuhusu elimu. Mungu awajazi kheri. Majongo yoṭ^{h}e yaliyomo humu ni yangu.

MAREJELEO

Ali, A.H.T. (2014). *Taashira na utendaji katika nyimbo za harusi za Waswahili kisiwani Zanzibar*. Tasnifu ya Uzamifu (haijachapishwa), Egerton University, Njoro.

Bakhtin, M. M. (1981). *Dialogic imagination: Four essays*. M. Holquist (mh.), C. Emerson & M. Holquist (waṭafsiri). University of Texas Press.

Bakhtin, M. M. (1986). *Speech genres and other late essays*. C. Emerson & M. Holquist (wah.). Imetafsiriwa ni V.W. McGee. University of Texas Press.

BAKITA. (2016). *Kamusi kuu ya Kiswahili*. Longhorn Publishers Limited.

Charles, L & Ochieng, D. (2023). Mapping the distribution of euphemisms across taboo themes in Swahili. Katika *Journal of Languages, Linguistics and Literary Studies 3*

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2258

(2), 62- 71. https://doi.org/10.57040/jllls.v3i2.439

Ferguson, S. (Oktoba 25, 2019). Does it hurt when your hymen breaks. Imesomwa: https://www.healthline.com/health/healthy-sex/does-it-hurt-when-your-hymen-breaks

Krapf, L. (1882). *A dictionary of Suahili language*. Trubner & Co.

Madan, A.C. (1903). *Swahili - English Dictionary*. Clarendon Press.

Matona, I. (2020, Agosti). Hongera mwanangu [video file]. Imetolewa: https://youtu.be/DTt4LFxRs2Q?si=K2-Wzei3T-OfUQtU

Mbaabu, I. (1985). *Utamaduni wa Waswahili*. Kenya Publishing & Book Marketing Co. Ltd.

Middleton, J. (1992). *The world of the Swahili: An African mercantile civilization*. Yale University Press.

Mohamed, A.M. & Mohamed, S.A. (2002). *Kamusi ya visawe*. East African Educational Publishers.

Mohamed, S.A. (2002). *Jicho la ndani*. Longhorn publishers Limited.

Mohamed, S.A. (2015). *Mhanga nafsi yangu*. Longhorn publishers Limited. Sacleux, C. S. (1891/1939). *Dictionnaire Swahili - Francais*. Institut d' Ethnologie.

Steere, E. (1919). *A handbook of the Swahili language as spoken at Zanzibar*. Society for Promoting Christian Knowledge.

Strobel, M. (1979). *Muslim women in Mombasa 1890-1975*. Yale university Press.

Taylor, W. E. (1891). *African aphorisms*. Society for Promoting Christian Knowledge.

Timammy, R. (2002). *Mombasa Swahili women's wedding songs: A stylistic analysis*. Tasnifu ya PhD (Haijachapishwa), University of Nairobi, Nairobi.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Oxford University Press.

Walibora, K. (2016). *Nasikia sauti ya mama*. Longhorn publishers Limited.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.